Habari uk 1,4 uk 17.

# majira

GAZETI HURU LA KILA SIKU
www.timesmajira.co.tz
ISSN 0856-5086 ■ NA. 9297 • VOL. II/8398
Alhamisi 21 • JANUARI • 2021
BEI: TSHS 1000/KSHS 60

Taasisi zahimizwa kuendeleza kutumia kiswahili UK. 9

# Wizara yapewa rungu kushughulikia NARCO

- **Yatakiwa kuongeza idadi ya mifugo kwenye ranchi zake, vinginevyo maeneo ambayo haiyatumii wapewe wafugaji wengine kwa gharama nafuu** UK. 4



Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa akizungumza wakati alipofungua mkutano wa wadau wa zao la mkonge kwenye ukumbi wa hoteli ya Regal Naivera jijini Tanga, jana. (Picha na Ofisi ya Waziri Mkuu)

## Halmashauri zinazolima mkonge zatakiwa kuandaa miche

**Na Yusuph Mussa, Tanga**

WAZIRI Mkuu Kassim Majaliwa, ameagiza kila halmashauri yenye wakulima wa mkonge kuandae vitalu vya miche ya zao hilo, lenye ukubwa wa ekari... Inaendelea Uk. 16

## DED ataja siri kushuka kwa elimu Mkalama

**Na Jumbe Ismailly, Mkalama**

TATIZO la mdondoko kwa wanafunzi wa shule za msingi katika Halmashauri ya wilaya ya Mkalama, mkoani Singida bado ni kubwa kutokana na wanafunzi... Inaendelea Uk. 4

# Maendeleo kufanyika kwa kuzingatia mipango Miji Uk. 4

Scanned with CamScanner

# Wizara yapewa rungu kushughulikia NARCO

**Na Mwandishi Wetu, Kagera**

RAIS John Magufuli ameiagiza Wizara ya Mifugo na Uvuvi kuhakikisha Kampuni ya Ranchi za Taifa (NARCO) inaongeza mifugo katika ranchi zake zote, na kwa maeneo ambayo haiyatumii wapewe wafugaji wengine na kwa gharama nafuu.

Rais Magufuli alitoa agizo hilo juzi akiwa wilayani Kagera wakati akizindua kiwanda cha kuchakata maziwa cha Kahama Fresh ltd kinachomilikiwa na Jossam Ntangeki.

Alisema zipo taasisi za Serikali zenye maeneo makubwa ya ufugaji kama NARCO, lakini ng'ombe hawaongezeki. "Sasa sijui kwa nini ng'ombe hawaongezeki, wakati huyo mwekezaji ana eneo dogo, lakini ana ng,ombe wengi?" Alihoji Rais Magufuli.

Alisema kama NARCO haina wataalam waende wakajifunze kwa mwekezaji wa Kahama Fresh.

Alimpongeza, Ntangeki kwa uwekezaji huo na alitoa wito kwa Watanzania kujitokeza kuwekeza katika ufugaji na uzalishaji wa maziwa kwa kuwa mahitaji ya maziwa kwa Tanzania ni makubwa kuliko uzalishaji uliopo licha ya kuwa nchi ya pili kwa idadi kubwa ya mifugo barani Afrika.

"Kati ya watu wanaoteseka nchini ni pamoja na wafugaji, kwani kila wanapokwenda wamekuwa wakifukuzwa na kuna wakati miaka ya nyuma zilifanyika operesheni za kuwaumiza wafugaji," alisema.

Alipongeza mwelekeo wa wizara wa kuijenga sekta ya mifugo, kwani vikianzishwa viwanda vingi hawatakuwa na sababu ya kuhamahama, bali watauza maziwa yao na wawekezaji watatengeneza ajira.

Alimpongeza mwekezaji kwa kuanzisha kiwanda cha maziwa kuliko ya kutegemea maziwa ya kutoka nje ambayo haijulikani yametengenezwaje.

"Kwa hiyo tukiendeleza sekta hizi za Watanzania wenzetu hatuwezi kudanganywa, huyu hawezi kutudanganya au kutuwekea maji," alisema Rais Magufuli.

Aliwaomba wafugaji kushikamana, kwani sekta ya mifugo niendelevu kama ilivyo sekta zingine katika kuchangia pato la taifa.

**Wakati huo huo,** Magufuli juzi alishuhudia utiaji saini wa mikataba ya uwekezaji kati ya Serikali ya Tanzania na kampuni ya LZ Nickel Limited juu ya uchimbaji wa madini ya Nickel yaliyopo Kabanga katika Wilaya ya Ngara Mkoani Kagera.

Hafla ya utiaji saini mikataba hiyo ilifanyika Mjini Bukoba na kuhudhuriwa na viongozi mbalimbali wakiwemo Mawaziri na Naibu Mawaziri, Katibu Mkuu Kiongozi, Balozi John Kijazi, Balozi wa Uingereza hapa nchini, David William Concar, Makatibu Wakuu na Naibu Makatibu Wakuu, Mwanasheria Mkuu wa Serikali Prof. Adelardus Kilangi, viongozi wa Dini, viongozi wa vyama vya siasa na viongozi wa Mkoa wa Kagera wakiongozwa na Mkuu wa Mkoa huo, Brig. Jen. Marco Gaguti.

Kwa upande wa Tanzania mkataba huo ulisainiwa na Waziri wa Madini, Doto Biteko na Msaili...

# DED ataja siri kushuka kwa elimu Mkalama

**Na Jumbe Ismailly, Mkalama**

TATIZO la mdondoko kwa wanafunzi wa shule za msingi katika Halmashauri ya wilaya ya Mkalama ...

2020,2,710 sawa na asilimia 54.85 walichaguliwa kuendelea na masomo.

Kwa mujibu wa Mhandisi Sanga kutokana na takwimu hizo mwaka 2017 na waliotegemewa kufanya mtihani wa upimaji wa Taifa wa darasa la nne ni 9,024 wakiwemo wavulana 4,577 na wasichana 4,447 lakini ...

Scanned with CamScanner

HABARI Majira



# Ubora viwanda vya nyama waongeza kasi usafirishaji nyama nje

Na Mwandishi Wetu

KASI ya kusafirisha nyama kwenda nje ya nchi, imeongezeka kutokana na kuwepo kwa ubora wa viwanda vya nyama, ikiwa ni uwekezaji mkubwa uliopo jambo linalosababisha kuwa na nyama bora na salama kwa ajili ya matumizi ya binadamu na kukidhi soko la ndani na nje ya nchi.

Hayo yalisemwa na Kaimu Msajili wa Bodi ya Nyama Tanzania, Imani Sichalwe akiwa kwenye ziara ya kukagua mazingira ya usafirishaji wa nyama kutoka nchini kwenda nje ya nchi aliyoifanya mwishoni mwa wiki katika Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Mwalimu Julius Nyerere Jijini Dar es salaam.

Sichalwe alisema uwepo wa viwanda hivyo vya nyama vya kisasa nchini, ndio vinafanya kuwe na ithibati ya kupeleka nyama nje ya nchi ambapo kiwanda cha Tanchoice kilichopo Kijiji cha Soga wilayani Kibaha mkoani Pwani, chenye uwezo wa kuchinja mbuzi 4,500 kwa siku na ng'ombe 1,000 kwa siku moja ambapo kwa Januari 16 mwaka huu, kimepeleka mbuzi 2,000 waliochinjwa sawa na kilo 20,000 au tani 20 kwenda nchi za Oman na Kuwait.

"Kwa sasa kwa wiki kiwanda cha nyama cha Tanchoice kilichopo Kibaha mkoani Pwani, husafirishwa mbuzi waliochinjwa 6,000 sawa na kilo 60,000 sawa na tani 60 kwenda Omani, Qatar na Kuwait na kwa wiki ijayo kiwanda kitaanza kupeleka nyama katika soko jipya la Hongkong. Kwa upande wa kiwanda cha nyama cha Eliya Foods Overseas Limited, kimeanza kupeleka nyama kwenda Oman mbuzi 1,874 sawa na tani 14.6," alisema.

Katika ziara hiyo Kaimu Msajili huyo wa Bodi ya Nyama alisema, ameridhika na namna shughuli nzima ya utaratibu unaofanywa kuanzia kushusha nyama kwenye gari, kuingiza katika vyumba maalumu vya kuhifadhia na kupooza pamoja na namna ya upakiaji wa nyama hizo kwenye ndege.

# Ubora viwanda vya nyama waongeza kasi usafirishaji nyama nje

**Na Mwandishi Wetu**

KASI ya kusafirisha nyama kwenda nje ya nchi, imeongezeka kutokana na kuwepo kwa ubora wa viwanda vya nyama, ikiwa ni uwekezaji mkubwa uliopo jambo linalosababisha kuwa na nyama bora na salama kwa ajili ya matumizi ya binadamu na kukidhi soko la ndani na nje ya nchi.

Hayo yalisemwa na Kaimu Msajili wa Bodi ya Nyama Tanzania, Imani Sichalwe akiwa kwenye ziara ya kukagua mazingira ya usafirishaji wa nyama kutoka nchini kwenda nje ya nchi aliyoifanya mwishoni mwa wiki katika Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Mwalimu Julius Nyerere Jijini Dar es salaam.

Sichalwe alisema uwepo wa viwanda hivyo vya nyama vya kisasa nchini, ndio vinafanya kuwe na ithibati ya kupeleka nyama nje ya nchi ambapo kiwanda cha Tanchoice kilichopo Kijiji cha Soga wilayani Kibaha mkoani Pwani, chenye uwezo wa kuchinja mbuzi 4,500 kwa siku na ng'ombe 1,000 kwa siku moja ambapo kwa Januari 16 mwaka huu, kimepeleka mbuzi 2,000 waliochinjwa sawa na kilo 20,000 au tani 20 kwenda nchi za Oman na Kuwait.

"Kwa sasa kwa wiki kiwanda cha nyama cha Tanchoice kilichopo Kibaha mkoani Pwani, husafirishwa mbuzi waliochinjwa 6,000 sawa na kilo 60,000 sawa na tani 60 kwenda Omani, Qatar na Kuwait na kwa wiki ijayo kiwanda kitaanza kupeleka nyama katika soko jipya la Hongkong. Kwa upande wa kiwanda cha nyama cha Eliya Foods Overseas Limited, kimeanza kupeleka nyama kwenda Oman mbuzi 1,874 sawa na tani 14.6," alisema.

Katika ziara hiyo Kaimu Msajili huyo wa Bodi ya Nyama alisema, ameridhika na namna shughuli nzima ya utaratibu unaofanywa kuanzia kushusha nyama kwenye gari, kuingiza katika vyumba maalumu vya kuhifadhia na kupooza pamoja na namna ya upakiaji wa nyama hizo kwenye ndege.

Scanned with CamScanner

funzi ana mahitaji yanayojitosheleza

# Mifugo ya wazazi kuuzwa kuwanunulia sare wanafunzi

SALVATORY NTANDU, KAHAMA

SERIKALI wilayani Kahama imesema ikibidi itauza mifugo ya baadhi ya wazazi wa watoto wanaosoma shule za msingi na sekondari watakaobainika hawana sare na mahitaji muhimu ya kimasomo.

Kauli hiyo ilitolewa juzi na Mkuu wa Wilaya ya Kahama, Anamringi Macha, wakati akizungumza na waandishi wa habari ofisini kwake kuhusu udahili wa wanafunzi wa darasa la kwanza na kidato cha kwanza.

Alisema hadi sasa uandikishaji na usajili wanafunzi unakwenda vizuri, lakini kuna baadhi ya wanafunzi wamepokelewa na kuanza masomo, huku hawajakamilishiwa mahitaji muhimu ikiwamo sare za shule.

"Tutatumia sheria kukamata na kuuza mifugo ya wazazi ambao watakaidi kuwanunulia watoto wao mahitaji ya shule, haiwezekani mzazi anamiliki mifugo zaidi ya 50 halafu watoto wake wanakwenda shule bila sare, madaftari na hata viatu hawana, tutaiuza kwa njia ya mnada mifugo hiyo na fedha zitatumika kununua vifaa hivyo," alisema Macha.

Macha alifafanua kuwa fedha zitakazobaki baada ya kuuza mifugo hiyo watakabidhiwa wazazi na uamuzi huo unatokana na jamii za wafugaji na wakulima katika wilaya hiyo kuwa na mwamko mdogo wa elimu.

"Mwaka huu tutawatumia wanasheria wetu wa serikali kuwabana wazazi ambao hawataki watoto wao wapate elimu, licha serikali kutekeleza sera ya elimu ya msingi bure kuanzia awali hadi kidato cha nne," alibainisha.

Mkazi wa Mtaa wa Nyakato, Florian Majembele, alisema hatua hiyo serikali itasaidia kuwakumbusha baadhi ya wazazi wajibu wao katika suala la elimu.

Kwa upande wake, Shija Masolwa, mkazi wa Mtaa wa Manzese, alisema baadhi ya jamii za wafugaji na wakulima hazithamini elimu badala yake hupenda watoto wao wajue kufuga na kulima, mtazamo ambao unapaswa kukosolewa kwa kuwapa elimu.

> **Tutatumia sheria kukamata na kuuza mifugo ya wazazi ambao watakaidi kuwanunulia watoto wao mahitaji ya shule, haiwezekani mzazi anamiliki mifugo zaidi ya 50 halafu watoto wake wanakwenda shule bila sare, madaftari na hata viatu hawana, tutaiuza kwa njia ya mnada mifugo hiyo na fedha zitatumika kununua vifaa hivyo**
>
> Mkuu wa Wilaya ya Kahama, Anamringi Macha,

Scanned with CamScanner

AFYA

KITIMOTO

# *Nyama iliyosheheni mashabiki wengi, daktari akiwapa vigezo*

Na Sabato Kasika

• Unataka kula? Zingatia mambo haya hapa



Nyama ya nguruwe ikiwa buchani. **PICHA ZOTE: MTANADAO**

NYAMA ya nguruwe katika zama za karibuni, imeingia katika orodha ya kupendwa sana katika sura ya kitaifa.

Kihistoria nchini ilijulikana baadhi ya mikoa kama Mbeya kulikofugwa na kuliwa kwa wingi, lakini kadri muda ulivyoenda, hasa kuanzia mwishoni mwa miaka 1980, ulaji uliongezeka, Dar es Salaam, ikiibuka mwenyeji.

Leo imefikia hadhi kuwa miongoni mwa mlo unaopendwa sana mijini, ambako si haba imejaa kwenye bucha na mishikaki yake imejaa kwenye 'vituo vya msaada' vingi, vinavyojumuisha baa, baadhi ya wateja wakiunganisha na mseto 'moja moto moja baridi.'

Umaarufu wa nyama hiyo, umesababisha ipatiwe majina mengi bandia, ikiwamo 'Noah' na 'Kitimoto', ambayo sasa ina hadhi ya msamiati pori, ikiwa rasmi kila kona.

### SHIDA ILIYOPO

Ulaji nyama hiyo inayowakonga walaji, pia ina upungufu wa kuzaa matatizo ya kuwa na magonjwa inajumuisha 'African Swine Fever' ambao ni minyoo ya tegu.

Ni aina ya maradhi yanayotajwa na wataalamu wa magonjwa ya mifugo kuwa mlaji nyama ya nguruwe anaweza kudhurika, iwapo itapikwa na kuliwa bila kuiva vizuri.

Utaratibu wa kitabibu wa kiserikali ni kwamba, kila penye mlipuko wa ugonjwa tegi unapowakumba nguruwe, serikali hupiga marufuku ulaji, uuzaji nyama yake hadi hali inapokuwa shwari, ndipo unaendelea.

Mtaalamu na mstaafu wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Dk. Sero Hassan Luwongo, anaueleza kuwa ni ugonjwa usiokuwa na chanjo wala tiba, bali nguruwe kuwekwa ndani ya karantini hadi uishe.

Katika mazungumzo yake na Nipashe, Dk. Luwongo anasema, ulaji wa nyama ya nguruwe isiyoiva vizuri, inamsababishia mlaji kukumbwa na ugonjwa wa kifafa.

Anafafanua kuwa nyama ya nguruwe inapokuwa na minyoo na haijaiva vizuri, inasababishia mlaji kupata uvimbe kwenye ubongo na ndipo inafuata uwezekano wa kupata kifafa.

Dk. Luwongo anasema uvimbe wa ubongo upo wa aina nyingi, akiufafanua: "Nguruwe ana magonjwa kama walivyo wanyama wengine ambayo yanatibika, yakiwamo ya kwato, lakini minyoo ya tegu inayoitwa African Swine Fever, haitibiki na ndiyo yenye madhara."

Anasema, nyama ya nguruwe ina minyoo ambayo ni wagumu kufa, hali inayotoa uwezekano wakaingia mwilini na kujenga uwezekano wa kufika kwenye ubongo, jambo linalojenga uwezekano wa madhara hayo.



Nyama ya nguruwe tayari kwa kuliwa.

> **"Virusi hivyo havina tiba wala chanjo. Njia pekee ni kupika nyama na kuhakikisha imeiva vizuri, pia ugonjwa unapolipuka, ni kupiga marufuku usafirishaji.**

"Virusi hivyo havina tiba wala chanjo. Njia pekee ni kupika nyama na kuhakikisha imeiva vizuri, pia ugonjwa unapolipuka, ni kupiga marufuku usafirishaji, ulaji wa nyama ili kuzuia ugonjwa usisambae,|" anasema.

### MLIPUKO NCHINI

Ni ugonjwa unaotajwa kuibuka kila mara nchini na mwaka 2017 ulitua katika wilaya za Kalambo mkoani Rukwa na Dodoma na kusababisha viongozi kupiga marufuku ulaji nyama ya nguruwe.

Pia hatua ya karibuni ni kwamba umetua wilayani Kahama Mkoa wa Shinyanga, unadaiwa kuua nguruwe zaidi ya 500 na serikali kupitia ofisi ya wilaya, alipiga marufuku uuzaji, usafirishaji na ulaji wa nyama ya nguruwe kwa muda usiojulikana hadi hali itulie.

Mkuu wa Wilaya, Anamringi Macha, anasema ni hatua ya kudhibiti kuenea maambukizo ya ugonjwa huo unaodaiwa kuua nguruwe kwa kasi wilayani kwake na wataalamu wetu wanaendelea kufanya utafiti kuhakikisha wanaudhibiti, ili kuzuia madhara zaidi yasijitokeze.

Aidha, Macha anawataka walaji nyama ya nguruwe wilayani mwake kuachana nayo hadi watakapotangaziwa na serikali, hivyo watumie mbadala wa nyama ya mifugo kama ng'ombe, mbuzi, kondoo na kuku kwa kuwa hawajaathiriwa na ugonjwa huo.

### KULIVYO DUNIANI

Utafiti uliofanywa na Shirika la Afya Duniani (WHO) na The International Agency for Research on Cancer unamtaja nguruwe ni mnyama, nyama yake inaliwa kwa wastani na asilimia 38 ya wakazi wote duniani.

Hata hivyo, anatoa kasoro kuwa nyama hiyo ina madhara makubwa, akitaja ni sumu ya anayoiita 'carcinogen' inayosababisha ugonjwa wa saratani.

Kwa mujibu wa watafiti hao wa WHO, wanaainisha pale kila siku mtui alapo gramu 50 ya nyama ya nguruwe, ana uwezekano wa kupata saratani kwa watani wa asilimia 18. Utafiti uliofanyika 1998 wa WHO, ulionyesha nyama ya nguruwe iliyopikwa kwa nyuzi joto 104C, bado zaidi ya nusu (asilimia 52.37) ya minyoo iitwayo 'trichinella worm' hawafi.

Hiyo ni minyoo ambayo inapoingia mwilini mwa binadamu, husababisha ugonjwa uitwao 'trichinosis' ambao dalili zake kwa mgonjwa zanajuimuisha homa kali; kichwa kuuma; kukosa nguvu; maumivu ya nyama za mwili; macho kuwa rangi ya pinki; kuvimba uso na kope; na kudhuriwa na mwanga.

WHO inatahadharisha namna kuwapo minyoo aina tofauti waitwao kitaaalamu ' Taenia solium' mlaji nyama anaweza kuipata isipopikwa vizuri na inasababisha matatizo ya mfumo wa fahamu na ndio chanzo cha maradhi ya kifafa.

Pia inaelezwa ni aina ya nyama yenye virusi vinayosababisha homa ya ini aina 'E' na kuna kuna wadudu wanaobaki ambao nao wana madhara tofauti mwilini kwa binadamu mlaji.

### FAIDA NA HASARA

Hadi sasa inaelezwa asilimia 30 ya wagonjwa wote duniani wenye kifafa huwa ni wanaoshambuliwa na minyoo hiyo ipatikanayo kwenye nyama ya nguruwe isiyoiva vizuri.

Inaelezwa kuwa watu milioni 50 duniani kote wenye kifafa ni walaji wa nyama ya nguruwe kwa namna tofauti kama vile soseji, au nyama iliyopikwa.

Pia kuna faida ikitajwa vitamini muhimu katika mwili wa binadamu; ambazo ni B1, B6 na B12 na walaji wanapata madini chuma, yanayowasaidia kuimarisha mifupa, huku magnesium inayosaidia mwilini mwa binadamu.

Mengine ya manufaaa ni viini lishe vya protini ya kutosha, ambayo inachangia kujenga mwili, pia mafuta yanayoufanya mwili kupata nguvu.

Nyama ya nguruwe inaingia katika orodha ya kuimarisha ngozi ya mlaji kuifanya iwe laini.

Scanned with CamScanner

husika kisha tunatafuta taarifa zake Nida

ya elimu ua sekondari kama inavyotakiwa ili kupata haki zao za msingi

kwetu

MWANANCHI UK

# SAMAKI: WAPO TAYARI

Mwanachama wa Chama cha Ushirika cha Ibanda Fish Dealers Society, Siraji Mbaze akiwa amemnyanyua samaki aina ya kayabo ambao hukaushwa juani. Samaki hao husafirishwa kwenda Jamhuri ya Kidemokrasia Kongo (DRC), Rwanda na Burundi. **Picha na Mgongo Kaitira**



Scanned with CamScanner


HABARI LEO UK 6.

al
o
ifa

husu kampuni
ya katika mfumo
korosho ambao
abadiliko
a pia.
deleza wajasiria-
wa kuwawezesha

ambao utaanza na
zania kuchakata
ali ya kujenga

o hilo ambalo
kika wa korosho
mlaka zinazo-
kulifanikisha ili



Rais John Magufuli akiwa na Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Mashimba Ndaki wakifunua kitambaa ikiwa ni ishara ya kuweka jiwe la msingi la mradi wa ujenzi wa kiwanda cha kusindika maziwa na vyakula vya mifugo cha Kahama Fresh mjini Karagwe unaoendeshwa na mwekezaji mzawa, Jossam Ntangeki juzi. (Picha na Ikulu).

## WAZO LANGU

Scanned with CamScanner

HABARI LEO UK 17

# JPM aishauri TADB kukopesha wafugaji

Na Diana Deus, Bukoba

RAIS John Magufuli amefurahishwa na utendaji kazi wa Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania (TADB) na kuitaka iendelea kukopesha wafugaji kutokana na kuwa moja ya sekta muhimu za kuinua uchumi wa nchi.

Rais Magufuli alisema hayo wakati akiweka jiwe la msingi la ujenzi wa kiwanda cha maziwa cha Kahama Fresh kinachojengwa na mwekezaji wa ndani katika kata ya Kihanga, wilayani Karagwe.

"Ninajua kuna ugumu wa kufikiria kuwa wafugaji hawakopesheki lakini naamini wafugaji wengi ni waaminifu."


"Mara nyingi mfugaji yuko tayari kufa yeye kuliko mfugo wake, hivyo moyo wa wafugaji upo katika mifugo yao na walio wengi hawawezi kukimbia na fedha za kilimo."

"Kwa dhati kabisa naipongeza Benki ya Maendelea ya Kilimo imeleta mabadiliko amkubwa kwa wawekezaji wa ndani, kama mnaweza kuwakopesha wafugaji tunaweza kuinua uchumi wetu kupitia mifugo," alisema.

Rais Magufuli alisema wafugaji hawawezi kukimbia na fedha za mkopo kwa sababu wengi hukaa kulinda mifugo yao.

"Wakazi wa Karagwe nataka niwaambie kuwa mifugo ni uchumi na tukijikita kufuga kisasa tunaweza kuchangia uchumi wetu," alisema.

Aidha, Rais Magufuli alisifu uwekezaji wa kiwanda hicho na kuwataka wafugaji wa maeneo jirani kutumia fursa hiyo kujifunza ufugaji wa kisasa na kuuza maziwa yao kiwandani hapo ili kujiinua kiuchumi.



Aliwasisitiza wananchi kutumia maziwa kwa wingi kwani kiwango cha maziwa kinachotumiwa na mwananchi mmoja ni kidogo ikilinganishwa na viwango vinavyotakiwa na Shirika la Afya Duniani (WHO).

Mwekezaji wa kiwanda hicho, Josam Ntangireki alisema uwekezaji huo unathamani ya Sh bilioni tisa na kwamba ndani ya kiwanda hicho kutakuwa na kiwanda kingine cha kuchakata malisho ya mifugo ili kuepuka changamoto ya mifugo kutotoa maziwa wakati wa kiangazi kutokana na kukosa malisho.

Alisema anaishukuru serikali kwa kuanzisha TADB kwani imempatia mkopo wa Sh bilioni 2.2 haraka bila vikwazo vingi kama zilivyo benki nyingine.

Alisema kiwanda hicho kikikamilika kitatoa ajira kwa watu 400 na kuwa chachu ya ufugaji bora kwa mkoa wa Kagera, huku wafugaji wadogo wakitarajia kunufaika na kiwanda hicho kwa kuuza maziwa yao na kujipatia kipato.